
Toleo 21

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

*YALIYONUKULIWA KUTOKA KWA*

## URITHI WA UKRISTO WA MATUMIZI YA MUZIKI WA A KAPELA (AMBAO HAUTIMII ALA ZA MUZIKI) KATIKA IBADA ZA MUNGU



*na Harlan Sorrell*

Muziki unaotumia ala za muziki haukutumika katika ibada za Kikristo hadi wakati Kanisa la Kikatoliki lilipoacha dini ya kawaida; lakini hata Kanisa la Kikatoliki lilikubalisha matumizi ya ala za muziki kanisani shingo upande. Nalo kanisa la Kiothodoksi-Kiyunani (Greek Orthodox) kamwe halikukubali vyombo vya muziki kutumika katika ibada zao, na ni dhahiri kwamba hata wabadilishaji wa dini (wa madhehebu ya Kiprotestanti) waliondoa vyombo hivyo kutoka kwenye ibada zao.

Neno *a kapela* ni neno la Kitaliano linalotokana na maneno mawili ya Kilatini, *a* likiwa na maana ya "kulingana na," na *kapela* likimaanisha "kanisa ndogo." Hii ndiyo sababu kamusi ya kizungu ya Webster inatoa maana ya *a kapela* kuwa ni "kulingana na mtindo wa muziki wa kanisa au kanisa ndogo; hasa kwenye mitindo ya kale, bila matumizi ya ala za muziki." Ni ukweli wa kihistoria kwamba huu ndio ulikuwa mtindo wa muziki wa kanisa tangu hapo nyakati za mitume.

Yule mhubiri wa kale Charles Spurgeon (wa kanisa la Kibaptisti) alisema kwa kweli na kwa uhakika kwamba ala za muziki "huwa kizuizi badala ya kuwa msaada wakati watu wanamsifu Mungu." Sauti ya muziki ya kupendeza sana ambayo ishawahi kusikika duniani ni ya watu wa Mungu wakipaza sauti kwa pamoja na kwa nia moja na huku tanakali zao za sauti zikilingana na uimbaji ambao umeimbwa ndani ya Roho. Muziki kama huo huwa ndio mdundo wa mbinguni na ndio huwavutia na kuchangamsha watu wenye roho safi, na pia kufanya wenye dhambi kuwa makini na kuisikia Injili.

Watu wote wanaojifunza Maandiko na historia ya kanisa kwa undani hutambua ni kwa nini kanisa la mitume halikutumia ala za muziki na ni kwa nini Wakristo wa dhehebu la Anabaptisti na wabadilishaji wa dini kama vile Martin Luther, Yohana Wesley, D.S. Warner na wengine wengi walipinga matumiza ya ala hizo katika *ibada* za kiroho. Wao walitumia ala za muziki katika uundaji wa nyimbo zilizoandikwa, au katika uimbaji wa nyimbo za kujifurahisha au kufurahisha jamii, lakini wakapinga sana matumizi ya ala hizo katika ibada za Mungu kwa maana walielewa kanuni ambayo imeandikwa katika Yohana 4:23-24 na Matendo ya Mitume 17:24-25, n.k. kwa maana kwa watu hawa maana ya Mkristo kumwabudu Mungu ni yeye kuruhusu *mtu wake wa ndani* kujitokeleza, iwe ni kwa njia ya maombi, mahubiri, au wimbo. Kama ambavyo historia imenena kuhusu Wakristo wa kale wao walikuwa "wa kiroho sana hivi kwamba hawangebadilisha ala ambazo hazina uhai au kuzitumia eti ndio ziandamane na sauti ya mwanadamu" (*Ensaklopidia ya Kikatoliki*. X, 651). Hakuna mziki ulio na urembo mwingi duniani kama ule wa kuunganishwa kwa sauti za wanadamu kwenye tanakali zile nne za

*(Endelea katika Ukurasa 2)*

"Sauti ya muziki ya kupendeza sana ambayo ishawahi kusikika duniani ni ya watu wa Mungu wakipaza sauti kwa pamoja na kwa nia moja na huku tanakali zao za sauti zikilingana na uimbaji ambao umeimbwa ndani ya Roho."





Tahariri 3

Mafundisho ya Biblia: Muziki Unaotumika Katika Ibada 4

Muziki Unaotumika Katika Ibada 5

Maswali na Majibu 7

Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu 8

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

sauti kwa njia kamili. Lakini ni jambo la huzuni kwamba watu wengi katika dunia ya sasa hawajawahi kuwa na nafasi ya kusikia muziki huo wa ajabu ambao unafanana na muziki wa mbinguni. Huu ni muziki ambao huguza moyo wa mwanadamu na kumpa changamoto kuliko kitu kingine kile.

Katika kipindi tunachoishi ibada za kweli ambazo zinakubalika zinafanyika wakati ambapo Wakristo wameinuliwa na kukaa pamoja na Kristo huko mbinguni wakiwa ndani ya Roho. Ibada ya aina hii haiwezi kupatikana kwa njia ya sherehe au kwa kutumia vyombo bali hutokana na uhusiano kati ya roho ya mwanadamu na Roho wake Mungu. Ndiposa tunaimba, tunaomba, tunatabiri (kuhubiri) ndani ya Roho, huku tukiwa na mamlaka ya Agano Jipya inayosema kwamba tunaweza kuhusisha mambo haya yote katika ibada. Lakini kamwe hatuna mwongozo wowote katika Agano Jipya unaotwambia kwamba *tucheze* ndani ya Roho. Kwa kweli Roho Mtakatifu anaweza (tu) kupaka mafuta muziki ambao unatoka ndani ya roho na nafsi ya mwanadamu. Mungu hashughuliki au kufurahishwa na muziki ambao tunaweza kuunda kupitia kwa mikono ya mwanadamu, mikono ambayo pengine ina ustadi mkubwa. Shauku lake Mungu ni kusikia na kunusa mdundo na ubani wa nyimbo tamu zinazotoka mioyoni mwetu.

Kunao wale wanaojihisi kwamba kuondoa ala za muziki kutoka ibada zao kutaadhiri ibada zao. Lakini jambo hilo halitakuwa kweli ikiwa ibada zao zinaongozwa na kuwa na upako wa Roho Mtakatifu.Ukweli ni kwamba ibada huimarika wakati vyombo vya muziki havitumiki kanisani, na badala yake ibada hizo kufanywa kuwa ni ushirika wa kiroho kati ya watu wanaoabudu kwa njia ya Roho wa Mungu. Ni wakati huo ndipo tunaweza kusikia sauti ambayo Mungu anataka tusikie — utamu na umoja wa nyimbo ambazo zinatokana na mioyo ambayo imeunganishwa na Roho wake na kuwa na mdundo wa nyusi zilizo na uhai na pia kuwa na utukufu wa kiungu. Mungu hakuondoa utaratibu na sherehe za Agano la Kale ili kutuachia kitu ambacho ni hafifu zaidi. Badala yake Yeye alitupatia kitu ambacho ni bora zaidi. Matumizi ya muziki ambao hautumii ala za muziki (a kapela) katika ibada za Mungu haustahili kuchukuliwa kwamba ni kitu kigeni katika mambo ya ibada, bali ni urithi ulio na thamani kubwa ambao ulitokana na siku za kale za Ukristo, wakati ambapo Ukristo haukuwa umeingiliwa na mambo ya kidunia.

"Wakati mmoja Bwana aliishi katika hekalu
zilizoundwa kwa mikono ya wanadamu,
Na alikuwa na watu wa aina moja, wana wa Israeli;
Na huko Yerusalemu kwa njia za kawaida
Akaabudiwa na wao wenye haki wa kale."

*[D. O. Teasley]*

Lakini Mungu akawa na mpango bora zaida,
Wakati taratibu za kale zingepitwa na wakati [Waebrania 9:10],
Na sasa Yeye adumu katika sehemu za ndani za mioyo ya wanadamu,
Na ibada inayompendeza ni ile yauvumba unaotoka ndani ya mioyo yetu. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Mpeni Bwana utukufu wa jina lake; mwabuduni Bwana kwa uzuri wa utakatifu.* —Zaburi 29:2

Katika robo hii ya mwaka tutaendelea kujenga juu ya toleo la 18 lililohusu agano zile mbili ambazo Mungu alianzisha. Kwa sasa watu wa Mungu hawamtumikii kwa njia ya kimwili bali kwa njia ya roho. Matumizi ya ala za muziki ni jambo ambalo halikuwako katika ibada za kanisa wakati wa kanisa la Agano Jipya. Sauti zinazotoka kwenye ala hizo na ambazo hazina roho ndani yake hazimletei Mungu utukufu, kama jinsi ambavyo uchomaji wa mishumaa hauleti utukufu kwenye ibada. Badala yake Mungu hupendezwa na kile ambacho kinatoka kwenye kinywa cha mwanadamu ambacho kimetokana na moyo ulio mtakatifu na safi. Lakini kuna watu wengi ambao husema kwamba swala hili linategemea hiari yake mtu, na kwamba hili si jambo muhimu. Je, hii ni kusema kwamba tunaweza kuchoma ubani na kufuata mifano mingine ya ibada ambayo hupatikana katika Agano la Kale?

Mimi nishawahi kuwa katika ibada nyingi hapa Marekani na hata katika nchi za ng'ambo ambako watu hutumia ala za muziki kama sehemu ya ibada zao. Hata ingawa ala hizo hufurahisha mwili wa mwanadamu mimi sijawahi kupata mahali ambako ala hizo huongeza ubora wa hali ya kiroho ya ibada hizo. Badala yake kati ya watu ambao wako na shauku kubwa ya Mungu mimi nimengudua kwamba ala hizo za muziki zimekuwa kizuizi kwa Roho wa Mungu kufanya kazi yake katika ibada. Kuhusu muziki makusanyiko yaliyo madogo sana yanaweza kuhisi haja ya kutumia piano au kifaa kingine cha muziki ili kutia nguvu wimbaji wao. Lakini ni afadhali zaidi kuabudu kwa sadaka za midomo yetu kama tunavyoagizwa katika Neno la Mungu bila kutumia ala hizo za muziki.

Watu wengi hutetea matumizi ya ala za muziki katika ibada zao huku wakidai kwamba hili ni swala la kitamaduni. Lakini hata ikiwa matumizi ya ngoma (za kitamaduni) inaweza kuwa ni jambo ambalo limetokana na tabia za kitamaduni ambazo zinapendwa na watu ambao wamezaliwa katika utamaduni huo, kwa kweli si jambo ngumu mtu kutambua kwamba furaha hii inayoletwa na matumizi ya ala hizo ni furaha ya kimwili tu.

Pia kuna wale wanaodai kwamba watu watavutiwa kwa ibada na kuokoka kutokana na matumizi ya ala hizo za muziki. Lakini mtu mwenye msimamo kama huo huwa anadhihirisha upungufu wa kuelewa mambo ya kiroho. Kitabu cha Yohana 6:43-44 kinasema "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka." Kitu kile ambacho tunatumia kuwavutia watu ndicho ambacho wanavutiwa nacho. Ikiwa tutatumia mambo ya kimwili kuwavutia watu basi hatutakuwa budi kuendelea kutumia mambo ya kimwili ili kuendelea kuwavutia ndiposa wasiache kuja kanisani ili wasituache. Lakini Roho Mtakatifu anataka awe ndiye kivutio na ni Yeye tu ambaye anaweza kufanya watu kuwa na toba ya kiungu. Ni Yeye tu awezaye kuguza moyo wa mwanadamu.

Bwana ndiye mwanzilishi wa muziki na hiki ni kipawa cha ajabu ambacho Mungu alitoa kwa wanadamu. Watu wa Mungu wameamuriwa kuimba ili kumtukuza Mungu na kutiana nguvu. Lakini ala za muziki ni vitu hafifu na mbadala wa upako na uwezo wa Roho wa Mungu kati ya watu wa Mungu. Kama Roho wa Mungu hapaki mafuta ibada basi ibada hiyo huwa kitu chenye kuchosha na ambacho hakina uhai ndani yake. Basi si jambo la kushangaza kwamba bila Roho watu wanakuwa na shauku ya kuwa na ala za muziki ili wajaze pengo hilo. Lakini ni bora zaidi watu kuimba katika roho kama ambavyo tunafundishwa katika Neno la Mungu na kama ilivyokuwa katika kanisa la kwanza. Wimbaji wa a kapela ndio njia "kamili zaidi" na ambayo inahitaji kuwa ndio mazoea ya watu wa Mungu.

Mhariri, Michael Smith.

Julai 2017.

*Tutembelee www.thegospeltruth.org ili kujiandikisha na kupata jarida za mbele.*



## Aina na Mifano

Inayowakilishwa na Ala za Muziki

Kuna mengi ambayo tunaweza kujifunza tunapowaza kuhusu ala za muziki kama aina na mfano wa umoja unaoletwa na Roho Mtakatifu katika maisha ya watu wa Mungu. Wakati hekalu la Mfalme Sulemani lilipowekwa wakfu makuhani 120 walipiga tarumbeta wakiwa na umoja wa uimbaji huku wakimsifu na kumshukuru Mungu (2 Mambo ya Nyakati 5:12-14). Ndiposa utukufu wa Bwana ukashuka na kujaza hekalu. Katika siku ya Pentekoste wafuasi 120 wa Kristo walikuwa katika chumba cha juu wakiwa na umoja mwingi. Roho Mtakatifu akashuka na utukufu wake ukawajaa. Hapo ndipo wakafanyika vyombo vyenye utakatifu na vyenye kutimiza mapenzi yake Mungu.

# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Muziki Unaotumika Katika Ibada

**Somo la Biblia:** *Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.* —Yohana 4:23-24

**Muhstasari:** Ala za muziki zilikuwa zikitumika katika Agano la Kale wakati ambapo ibada zilikuwa zinafuata taratibu na sherehe za kimwili. Lakini msingi wa ibada za Mungu katika nyakati hizi zetu za Agano Jipya ni roho, na Mungu amewaagiza watu wake *wamwimbie* na siyo *kumchezea*. Uimbaji wa a kapela (usiotumia ala za muziki) ndio unalingana na biblia na pia unalingana na mazoea ya Kanisa la Mungu.

**I. Ala za Muziki katika Agano la Kale**

A. Mwanzo 4:21 Zilivumbuliwa na Yubali.
B. Mhubiri 2:8 Ya kuwafurahisha wanadamu.
C. Kutoka 15:20-21 Miriamu anacheza.
D. 2 Kumbukumbu ya Nyakati 20:27-28 Ilitumika kuonyesha furaha na ushindi.
E. 1 Samueli 10:5 Manabii wakiwa na ala za muziki.

**II. Mfalme Daudi na Ala za Muziki**

A. 1 Samueli 16:15-23 Mchezaji stadi. Aliondoa roho kutoka ndani ya Sauli.
B. Zaburi 33:1-3 Sifu kwa ala za muziki (Zaburi 150:5-6).
C. 1 Kumbukumbu ya Nyakati 15:15-16 Ala za muziki ambazo Daudi aliamua.

**III. Matumizi ya Ala za Muziki katika Ibada za Hekalu ni Jambo Ambalo Daudi Alianzisha**

A. 1 Mambo ya Nyakati 23:5 Daudi aunda ala za muziki kwa ajili ya matumizi katika nyumba ya Mungu (2 Mambo ya Nyakati 5:1).
B. 1 Mambo ya Nyakati 25:6 Jinsi ala za muziki zilivyokuwa kulingana na mpangilie wa Daudi.
C. 2 Mambo ya Nyakati 29:25-28 Ala za muziki zinatengwa na kutumika kulingana na amri ya Daudi (Ezra 3:10).

**IV. Manabii Wakemea Jambo Hilo**

A. Isaya 5:11-13 Muziki watumika katika sherehe za kimwili.
B. Amosi 6:1-5 "Ole wenu" yatolewa kwa wale ambao wanaunda ala za muziki kama alivyofanya Daudi (Amosi 5:21-24).

**V. Kiwango Kipya Katika Kipindi cha Agano Jipya**

A. Mathayo 5:17 Sheria imetimizwa.
B. Waebrania 10:1-9 Kiwango kipya.
C. Yohana 4:23-24 Wamwabuduo Mungu humwabudu kwa roho na kweli.
D. Matendo 17:22-25 Mungu haabudiwi kwa mikono ya wanadamu.

**VI. Mafundisho na Mazoea ya Agano Jipya**

A. Mathayo 26:30 Yesu na wanafunzi wakaimba wimbo.
B. Warumi 15:9 Kuimba ili kumtukuza Mungu.
C. 1 Wakorintho 14:15 Kuimba kwa roho na kwa uelewaji.
D. Waefeso 5:18-20 Kuimba tenzi na nyimbo za rohoni.
E. Wakolosai 3:16 Kuimba zaburi, nyimbo, na tenzi za rohoni.
F. Waebrania 2:12 Kuimba sifa.
G. Waebrania 13:15 Kutoa sadaka za sifa kutoka kinywani.

**VII. Ibada za Kidunia**


A. 2 Timotheo 3:1-5 Wapenda anasa.
B. 1 Yohana 2:15-17 Usiupende ulimwengu.

**VIII. Kuabudu kwa Njia ya Kiroho**

A. Warumi 12:1-2 Kutoishi kulingana na dunia.
B. 1 Petro 2:5 Kutoa sadaka za kiroho.

**Tamati:** *Mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.* —Wakolosai 3:16.

# Muziki UNAOTUMIKA KATIKA IBADA



"Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu" (Yohana 4:23). Hayo ndiyo maneno ambayo Yesu alimwambia mwanamke Msamaria pale kwenye kisima. Maneno hayo yaliashiria kwamba sasa mabadiliko yalishafika na kutoka hapo ibada ya kweli itafanywa kwa njia na hali tofauti.

## Shauku la Kufanyika kwa Ibada za Kweli

Kabla ya wakati wa Yesu ibada zilikuwa za kitamaduni na za kisherehe tu. Watu wa Mungu walidumisha siku fulani kuwa takatifu, wakatoa sadaka zao, wakachoma ubani, wakafuata tamaduni kuhusu viwango vya usafi, wakacheza ala za muziki katika ibada, na mambo mengine mengi kama hayo. Lakini Kristo alipokuja Mungu hakutosheleka na ibada za kimwili bali alitaka kuwe na ushirika wa kiroho wa moyo wa mwanadamu kupitia kwa uwepo wake Roho Mtakatifu. Basi ingawa hata katika siku hizi zetu kungali na ibada sisizo za kweli, Mungu bado anawatafuta watu wa kumwabudu kwa kweli.

Kiasi kikubwa cha ibada za kisasa za Kikristo zinahusisha ala za muziki. Lakini inahitaji kuwa ni shauku la wana wa Mungu kwamba wawe wenye "kumwabudu Mungu kwa kweli" na kufanya mambo ambayo yanalingana na utakatifu na ambayo yanamletea Mungu heshima kubwa, utukufu, na kufanya watu kumsujudu Yeye. Wakati wa ibada unahitaji kuwa wakati ambao Mungu anatukuzwa na ni wakati unahitaji kutumiwa kuwapa waumini nguvu kwa mambo ya kiroho. Basi je, ikiwa hiyo ndiyo sababu inayofaa ya kufanyika kwa ibada, Mungu anawezaje kuabudiwa kwa njia bora kupitia kwa matumizi ya ala za muziki?

Kuna mambo mengi ambayo Mungu hakuyataja katika Biblia na badala yake alitupatia kanuni za kufuata. Kwa njia ya ushahidi wa kihistoria na kwa njia ya mtazamo wa mambo kwa umakini ni jambo lililo wazi kwamba kulingana na Maandiko na kupitia kwa Roho Mtakatifu matumizi ya ala za muziki silo jambo linalojenga ibada za kiroho katika wakati huu wa neema.

## Chanzo cha Ala za Muziki

Katika Mwanzo 4:21 tunaambiwa kwamba Yubali (ambaye alikuwa ni uzawa wa Kaini) alikuwa ndiye " . . . baba yao wapigao kinubi na filimbi." Uzao wa Kaini ulijulikana katika Maandiko kuwa ni "wana wa wanadamu" kwa maana wao hawakumfuata Mungu kama walivyofanya baadhi ya uzao wa Sethi ambao walijulikana kama "wana wa Mungu." Ni jambo la kustajabisha kwamba ala za muziki ziliundwa na watu wasiomcha Mungu na ambao hawakuwa makini kumpendeza Mungu. Hata ingawa si vibaya kutumia ala za muziki kwa ajili ya makusudi fulani au katika hali fulani, ukweli wa mambo ni kwamba adui yetu ametumia ala za muziki katika vizazi tofauti ili kuwapeleka watu mbali na Yeye ambaye anaweza kuwahudumia mioyoni kwa njia ya kweli na ambaye ndiye anaweza kupatia roho za binadamu amani ya kweli mioyoni mwao. Mfalme Sulemani alikiri na kusema kwamba yeye alikusanya dhahabu na fedha na hata waimbaji, "Nikajipatia waimbaji, waume kwa wake, nao wale ambao wanadamu wanawatunuka" (Mhubiri 2:8); lakini hata ingawa alijipatia hayo yote yeye alisema kwamba "yote ni ubatili na kujilisha upepo" (2:11). Hata ingawa sauti za ala za muziki zinaweza kumtubuisha mwanadamu, kumtuliza, na kumpatia faraja ya kiakili, kamwe haziwezi kumletea mwanadamu utakatifu.

*(Endelea katika Ukurasa 6)*

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)*

## Matumizi ya Ala za Muziki katika Agano la Kale

Ala za muziki zilitumiwa na watu wa Mungu katika Agano la Kale kwa viwango tofauti tofauti. Baada ya kuvuka Bahari ya Shamu Miriamu, ambaye alikuwa dada yake Aroni, alichukua tari mikononi mwake na kucheza pamoja na wanawake wale wengine (Kutoka 5:20-21) huku wakidhihirisha furaha na sifa zao kwa Bwana kwa njia ya kimwili. Ala za muziki zilitumika wakati wa ushindi wa majeshi vitani (2 Kumbukumbu ya Nyakati 20:27-28) na hata tarumbeta zilitumika kati ya watu wa Mungu kama ishara na mwito wa kufanyika kwa ibada kwa Mungu. Mfalme Sauli naye alikutana na kundi la manabii wakishuka kutoka mahali pa juu huku wakiwa wamebeba ala za muziki (1 Samueli 10:5). Naye nabii Elisha alisema aletewe mpiga kinubi ili amchezee (pengine ili kutuliza akili zake) kabla yake kutoa unabii kwa kuongozwa na Bwana (2 Wafalme 3:14-15). Lakini hata ingawa ala za muziki zilitumika hivyo ni muhimu kuzingatia kwamba ala hizo hazikutumika katika ibada za hema la makutano. Hata ingawa Mungu alisema wazi wazi jinsi *hema la makutano* lilihitaji kuundwa, na kusema fenicha zilizokuwa zitumike humo, na hata akasema kuhusu taratibu za dhabihu na ibada zake, ala za muziki kamwe hazikutumika katika ibada zilizofanywa humo.

"Ala za muziki hazikutumika katika ibada rasmi hadi wakati wa Daudi; na pia kwamba kila wakati Maandiko yakisema kuhusu ala za muziki yanasema wazi wazi kwamba ala hizo ziliamuriwa au kuwekwa wakfu kutokana na amri ya mfalme."



## Daudi —Ambaye Alipenda Muziki

Hata katika ujana wake Mfalme Daudi alikuwa mchezaji kinanda stadi. Wakati Mfalme Sauli aliandamwa na roho mbaya Daudi alimchezea, naye Sauli akapata tulizo, na roho mchafu akamwondoka (1 Samueli 16:15-23). Huu ni ushahidi wa nguvu za kimuziki. Muziki unaweza kuadhiri roho ya mwanadamu kwa njia ambayo maneno peke yake hayawezi. Hata ingawa matumizi ya ala za muziki yanaweza kuondoa shida na matatizo ya mwanadamu kutoka akilini mwake, jambo hili ni la kimwili na haliwezi kumletea mwanadamu mabadiliko ya kudumu.

Daudi alikuwa mtu mpenda muziki na pia alipenda ala za muziki ambazo ndizo ziliunda muziki huo. Sanduku la agano lilipohamishwa lilihamishwa "kama vile Musa alivyoamuru, sawasawa na neno la Bwana" (1 Mambo ya Nyakati 15:15-16); lakini Daudi alimwambia kiongozi wa Walawi kuchagua watu ili waimbe kwa kutumia ala za muziki. Hata ingawa jambo hilo halikuamuriwa na Mungu ilikuwa ishara ya ustadi wa Daudi kwa mambo ya muziki. Nacho kitabu cha Zaburi kimejaa maneno ya Daudi ya kutoa sifa na ambayo pia yanatilia maanani matumizi ya ala za muziki katika tendo la kumsifu Bwana (Zaburi 150:1-6)—"Mwimbieni wimbo mpya, pigeni kwa ustadi kwa sauti ya shangwe" (Zaburi 33:3).

## Mfalme Daudi Aamuru Ala za Muziki Zitumike

Mfalme Daudi aliunda ala za muziki kwa ajili ya matumizi katika nyumba ya Mungu (1 Mambo ya Nyakati 23:5). Hata ingawa ala za muziki hazikutumiki katika *hema la makutano* Maandiko yanasema wazi wazi kwamba waimbaji na wacheza ala za muziki walichaguliwa kwa ajili ya ibada za *hekalu* "wakiwa wanaamriwa na mfalme" (1 Mambo ya Nyakati 25:6). Walawi waliwekwa hekaluni "kama alivyoamuru Daudi" wakiwa na ala za muziki "vya Daudi mfalme wa Israeli" (2 Mambo ya Nyakati 29:25-28). Baada ya kuharibiwa kwa hekalu ya Sulemani na hekalu jipya likajengwa baada ya uhamisho wa Babeli, Ezra 3:10 inasema kuhusiana na Walawi kwamba walitumia ala za muziki kumsifu BWANA "kama alivyoagiza Daudi, mfalme wa Israeli." Hata ingawa ibada wakati huo ilikuwa ya kisherehe na pia haikuwa ya kiroho, tunahitaji kuelewa kwamba ala za muziki hazikutumika katika ibada rasmi hadi wakati wa Daudi; na pia kwamba kila wakati Maandiko yakisema kuhusu ala za muziki yanasema wazi wazi kwamba ala hizo ziliamuriwa au kuwekwa wakfu kutokana na amri ya mfalme.

## Manabii Watangaza "Ole Zao"

Nabii Isaya alitangaza ole zake kwa wale waliokunywa mvinyo kali, wenye kufanya sherehe ambako ala za muziki zilitumika lakini ambao hawakumtilia Bwana maanani. Nabii Amosi naye alikemea watu wa Mungu kwa njia ya moja kwa moja: "Ole wao wanaostarehe katika Sayuni, na hao wanaokaa salama katika mlima wa Samaria, . . . ninyi mnaoimba nyimbo za upuzi pamoja na sauti ya vinanda, na kujifanyizia vinanda vya namna nyingi, kama vile Daudi" (Amosi 6:1-5). Mungu alidhihaki sikukuu zao na akaacha kukubali sadaka zao: "Niondoleeni kelele za nyimbo zenu; kwa maana sitaki kuzisikia sauti za vinanda vyenu" (Amosi 5:21-24). Hata ingawa ala za muziki ambazo Daudi alizindua zilifanya kuwe na wimbaji mzuri na mtamu ambao uliweza kuguza hisia za wanadamu vifaa hivyo havikufanya wana wa Israeli kuwa na uhusiano wa kiroho na Mungu. Ndiposa mwandishi mmoja akauliza: "Kama vitu ambavyo viliundwa na mwanadamu zilikosa kuleta matunda ya kiroho wakati wa sheria, je, twawezaje kutarajia vifaa hivyo kuleta mazao mazuri ya kiroho wakati huu wa agano jipya?"


## Agano Jipya Linaanzisha Ibada za Kiroho

Sheria ikatimizwa (Mathayo 5:17) na njia ya utakatifu wa kweli na haki ikapatikana kupitia kwa Kristo. Agano la kwanza likaondolewa ili Yesu "alisimamishe la pili" (Waebrania 10:1-9) na akakamilisha kile ambacho sheria haingeweza kukamilisha. Maisha mapya ndani ya Kristo yakabadilisha tabia na ibada za wana wa kweli wa Mungu. Sasa hakukuwa tena na maagizo ya ibada za kimwili na badala yake kulikuwa na ushirika wa kiroho ambao huweka mtu huru bila kizuizi cha kimwili. Ndiposa mtume Paulo akahubiri katika kilima cha Mars huko Athene na kutangaza kwa ujasiri mwingi kwamba Mungu "hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono; wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu cho chote" (Matendo 17:22-25). Mungu kamwe hangeabudiwa wala kutukuzwa kwa kazi au ustadi wa mikono ya wanadamu na wala hangedumu katika hekalu zenye urembo mwingi ambazo aliundiwa na wanadamu au ambazo ziliundiwa miungu ya uongo. Mungu ni roho na yeye huabudiwa kwa ukweli na wale ambao Yeye alishawapa uhai na uzima. Kusema kweli mwanadamu alikuja ulimwengu akiwa ameandaliwa vya kutosha ili aweze kumwabudu Mungu na yeye hahitaji chochote zaidi ya maisha na pumzi zake ili kuweza kujitoa kama kifaa chenye utakatifu kwake Mungu.

## Mwili Wapingana na Roho

Katika Agano la Kale ibada kwa Mungu ilikuwa ni ya kimwili na ya kufuata sheria kulingana na ilivyoandikwa, lakini sasa ibada zote ambazo zinakubalika ni zile za Roho. Ibada za kweli za kiroho zinafanyika wakati ambapo ibada za kimwili zinazofanywa kwa njia ya sadaka, uchomaji ubani, na muziki wa vifaa visivyo na uhai ndani yake vimekomeshwa. Agano Jipya imetoa njia mpya ya ibada ambayo inafaa zaidi na ambayo ndiyo Kristo alifuata na kufuatwa pia na kanisa la kwanza. Baada ya sherehe za Pasaka Yesu na wanafunzi wake "waliimba wimbo" (Mathayo 26:30). Katika Agano Jipya hamna muziki wa Daudi au hata ala za muziki za Yubali. Kwa sasa Mungu hafanyiwi ibada kwa sauti zinazotokana na vyombo ambavyo vimeundwa na mwanadamu na badala yake Yeye huabudiwa kupitia kwa urembo wa utakatifu wa kweli – kitu ambacho hakiwezi kuundwa kwa njia ya talanta za kibinadamu. Warumi 15:9 inasema "nitaliimbia jina lako." Naye mtume Paulo anatoa mwongozo kwa kanisa la Korintho kwamba waimbe kwa roho na pia kwa akili (1 Wakorintho 14:15). Mtu haweze kuelewa chochote kutokana na ala za muziki bali uelewaji wote hutokana na moyo na midomo ya wale ambao wamehesabiwa haki. Kanisa la kwanza halikupewa maagizo ya kucheza ala za muziki ili kumsifu Bwana bali waliambiwa (mara nyingi) kwamba "waimbe sifa" (Waebrania 2:12). "Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu" (Waebrania 2:12). Nao Wakolosai walihimzwa kufunza na kuhimizina "kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu" (Wakolosai 3:16).

> "Kama vitu ambavyo viliundwa na mwanadamu zilikosa kuleta matunda ya kiroho wakati wa sheria, je, twawezaje kutarajia vifaa hivyo kuleta mazao mazuri ya kiroho wakati huu wa agano jipya?"



## Muziki Unaotumia Sauti za Mwanadamu Ndio Umeruhusiwa katika Agano Jipya

Agano Jipya halipingi matumizi ya ala za muziki katika ibada (kwa njia ya moja kwa moja), lakini pia hamna ruhusa ambayo imetolewa hapo

*(Endelea katika Ukurasa 8)*

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 7)*

ikihalalisha matumizi ya vyombo hivyo, kama ambavyo hakujatolewa ruhusa ya uchomaji wa ubani au uwashaji wa mishumaa. Mazoea na mafundisho ya Agano Jipya na ya Agano ya Kale kuhusu ibada ni jambo ambalo ni dhahiri kabisa, na sio vizuri watu kuchukulia kwamba jambo fulani limeruhusiwa wakati ambapo ruhusa ya jambo hilo haijatolewa. Sio tu kwamba Neno la Mungu halisemi chochote kuhusu matumizi ya ala za muziki katika Agano Jipya bali pia Agano hilo limewaamuru watakatifu kuimba na kufanya sauti za nyimbo mioyoni mwao. Wao wanaambiwa "tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake" (Waebrania 13:15). Muziki unaofanywa na sauti za wanadamu ndio muziki wa pekee ambao umeruhusiwa na Mungu katika ibada za Kikristo.

## Kama Mambo Yalivyokuwa Katika Kanisa la Mwanzo

Historia na Maandiko yamedhihirisha wazi kwamba kanisa la mwanzo liliabudu kwa kuimba na hakukuwa na matumizi ya ala za muziki katika mashirika yao. Tazama maneno yafuatayo kama yanavyonukuliwa kutoka kwa watu tofauti tofauti:



"Matumizi ya muziki silo jambo ambalo lilipokelewa katika makanisa ya mwanzo ya Kristo kama ambavyo matumizi hayo yalipokelewa na Wayahudi, Wakristo walikuwa wakiimba nyimbo za kawaida" (Justin Martyr 139 BK—Baada ya Kristo).

"Ni ala moja tu ambayo tunatumia yaani Neno la Mungu, ambalo kupitia kwake tunamheshimu Mungu. Kwa sasa hatutumii zaburi za kale, tarumbeta, ngoma au filimbi" (Klementi wa Iskanderia 153-217 BK).

"Konsati ya kimuziki ya kutumia zeze na kinanda ni ya Apolo, Muse na Makuri ambao ndio waliunda ala hizo; lakini sisi ambao ni Wakristo tunachukia mambo hayo kwa chukizo kuu ambalo hata waundaji wa vyombo hivyo wanastahili kuchukiwa nalo na kudhihakiwa kwa kiwango kikubwa kama hicho" (Tetuliani hapo mwendo wa 200 BK).

"Ala za muziki hazistahili kutumiwa na Wakristo" (Yohana Krisostomu 345-407 BK).

"Muziki ni jambo ambalo lilikuwako kanisani hata wakati wa mitume, lakini ala za muziki hazikuwa zikitumika" (Yusufu Bingham. *Works*. Vol. III, ukur. 137).

"Hamna shaka kwamba hapo mwanzo kila mahali muziki wa ibada za Mungu ulikuwa ule wa sauti za wanadamu" (Emili Naumani. *The History of Music*. Vol. I, ukur. 177).

"Shirika la Wakristo walikuwa na maoni yanayofanana na hayo, kwamba kutokana na maandishi ya mitume na wale waliofuata mitume: ala za muziki zilichukuliwa kuwa ambazo hazifai kwa ajili ya ibada za kidini; maandishi hayo ya Kikristo yamelaani kwa njia ya wazi kabisa uchezaji wa ala hizo za muziki. Mwanzoni nyimbo peke yake ndizo zilichukuliwa kuwa zinastahili kutumika ili kuwawezesha watu kumkaribia Mungu" (*New Oxford History of Music*. Vol I, ukur. 135).

"Lakini ni uimbaji peke yake na sio uchezaji wa ala za muziki ndio uliruhusiwa katika kanisa la kwanza" (Hugo Leichtentritt).

"Muziki ambao walitumia ulidhihirisha roho ya dini, roho yenye unyamavu wa ndani. Muziki wote ambao walitumia katika ibada zao za mwanzo ulikuwa wa kutumia sauti za wananadamu" (F. L. Humphrey. *Evolution of Church Music*).

"MIMI SINA SHIDA NA ALA ZA MUZIKI KATIKA MAKANISA YETU MRADI SIZIONEKANI WALA KUSIKIKA."
— YOHANA WESLEY (1703-1791)

## Ala za Muziki Zinaanza Kutumika katika Kanisa Katoliki

Ni katika karne ya 5 au 6 ndipo matumizi ya ala za muziki yalianzishwa kwa kiwango fulani katika kanisa Katoliki. Lakini ala hizo hazikuingizwa kanisani kwa kiwango kikubwa hadi hapo karne ya 16. Kulikuwa na kundi kubwa la watu waliopinga matumizi ya ala za muziki katika mkutano mkubwa wa Trent (Counsel of Trent) wa hapo mwaka 1545 hivi kwamba karibu mkutano huo upige marufuku kabisa matumizi ya ala hizo (*Schaff-Herzog Encyclopedia*. II, 1702). Na kwa miaka mingi baadaye wabadili wa dini za kiprotestanti hawakukubalisha matumizi ya ala za muziki katika ibada zao. Hata ingawa katika siku zetu litakuwa jambo la kushangaza kuona watakatifu wakiimba muziki wa *a kapela*, matumizi ya ala za muziki ni jambo ambalo wahubiri hao walihubiri dhidi yake katika madhehebu yote makubwa ya Kikristo kwa miaka mingi.

## Wakristo wa Kisasa Wanakumbatia Matumizi ya Ala za Muziki



Hata hivi ziku za karibuni (kama katika karne ya 19) wengi wa viongozi wa Kikristo walikataa kutumika ala za muziki katika ibada zao huku wakiamini kwamba ala hizo hazikustahili kutumika katika ibada za Mungu. Baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Marekani (hapo mwaka wa 1865) mhudumu wa injili Benyamini Franklin alisema kwamba kati ya makusanyiko 10,000 ya Kikristo ya huko Marekani kulikuwa na idadi isiyozidi 50 ya ala za muziki ambazo zilitumika makanisani humo. Lakini matumizi ya ala za muziki yamesambaa kote toka wakati huo. Makanisa yanaonekana kushughulishwa sana na swala la kupata wafuasi wengi ili

*(Endelea katika Ukurasa 10)*

## MANENO YA WALE WALIOBADILI DINI . . .

"CHOMBO CHA KULAINISHA MUZIKI KATIKA IBADA (ORGAN) NDICHO ALAMA YA BAALI. KANISA KATOLIKI LILIAZIMA CHOMBO HICHO KUTOKA KWA WAYAHUDI."
—MARTIN LUTHER (1483-1546)

"Katika sherehe za kutoa sifa kwa Mungu matumizi ya ala za muziki ni jambo ambalo halistahili kuweko, kama tu vile ambavyo hatustahili kuchoma ubani, kuasha mataa, au kurudisha mambo mengine ya sheria kanisani, ambayo kwa kweli yalikuwa ni kivuli tu. Basi ni ujinga kwa wafuasi wa Papa (Mtakatifu) kuazima jambo hilo na mengine mengi kutoka kwa Wayahudi. Watu ambao wanapendezwa na sherehe za kimwili ndio wanaweza kupendezwa na kelele hizo; lakini ibada zetu zinahitaji kufanywa kwa njia rahisi ambalo ndilo jambo lililopendekezwa na Mungu kwa njia ya mitume na ambalo ndilo jambo linalomfurahisha zaidi."

— Yohana Calvin (1509-1564)
*Commentary on the 33rd Psalm*

"YEYE (D.S. WARNER) ALIFUNDISHA KWA NJIA YA WAZI KABISA NA KWA UWEZO MKUBWA NA AKAPINGA MATUMIZI YA ALA ZA MUZIKI KATIKA IBADA ZA MUNGU. HAKUNA KUSANYIKO HATA MOJA [LA KANISA LA MUNGU] AMBALO LILITUMIA ALA HIZO WAKATI WAKE."
—C. E. ORR (1844-1933)
*NOT A NEW MOVEMENT*

"Zaidi ya hayo mimi naamini kwamba matumizi ya ala hizo za muziki katika kanisa la Kristo silo jambo limeruhusiwa na Mungu na pia ni jambo lililo kinyume na mapenzi yake; kwa kweli matumizi hayo ni jambo linaloharibu roho ya kweli ya ibada za Mungu, na ni dhambi . . . mimi sasa ni mzee na kusema kweli nimehudumu injili kwa miaka mingi; na sasa natangaza kwamba kamwe sijawahi kusikia kwamba matumizi ya ala hizo yanaleta faida yoyote katika ibada za Mungu; na pia nina sababu ya kuamini kwamba ni jambo ambalo linaleta uovu mwingi. Mtazamo wa muziki kwa njia ya kisayansi ni jambo ambalo mimi nalitukuza na linalonipendeza; lakini matumizi ya ala za muziki nyumbani mwa Mungu ni jambo ambalo ni chukizo na kero kubwa. Jambo hilo ni matumizi mabaya ya muziki; na mimi nasema waziwazi kwamba napinga uharibifu wote unaoingizwa ndani ya ibada zinazofanywa kwa Mwanzilishi wa Ukristo."

—Adam Clarke (1762-1832)
*Commentary on Amos 6:5*

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 9)*

wawahudumie kwa njia ya kimwili, badala ya wao kuhudumu kwa njia ya kiroho. Kwanza kabisa umwili huu uliingia kanisani kupitia kwa chombo cha kulainisha muziki (yaani organ) na pia kwa njia ya piano, na kukua hadi kukawa na bendi na vikundi vya waimbaji ambao hutumia aina zote za ala za muziki. Muziki wa kidunia sasa umefanywa kuwa muziki wa makanisa yanayojitangaza kuwa ya Kikristo! Kizazi hiki kinapima sifa na ibada za Kikristo kulingana na ustadi wa kutumia ala za muziki, na kwa hivyo ni kizazi ambacho kina umwili mwingi. Hata ingawa ala za muziki zinaweza kuvuta hisia na roho ya mwanadamu, hizi ni nguvu za kimwili ambamo ndani mwake hamna ibada za kweli za kiroho.

## Ibada za Kiroho Zinahitajika

Bila kujali tabia au mazoea ya kitamaduni—iwe ni upigaji wa ngoma za Kiafrika, uchezaji wa vyombo vya kulainisha muziki (organ) huko Asia, kuweko kwa okestra au makundi ya wanamuziki huko Uropa, na hata bendi za Marekani – urahisi wa ibada za kiroho kanisani unahitaji kuwa ndio muhimu kuliko tabia au mapendeleo ya jamii ambayo inawazunguka Wakristo. Njia hii ya kimwili ya kufanya ibada ni ya kidunia na inaambatana na tamaa za kimwili, tamaa za macho, na kiburi cha maisha (1 Yohana 2:15-17). Kwa sababu ya kupenda ulimwengu makusanyiko mengi yameacha njia rahisi ya kufanya ibada za kiroho, jambo ambalo ndilo limefundishwa katika Maandiko, na ambalo ndilo lilifuatwa katika kanisa la mwanzo. Mtume Paulo alimkanya Timotheo "siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa . . . wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake" (2 Timotheo 3:1-5).

## Ibada Ambazo Zinaongozwa na Roho Mtakatifu

Hata katika siku zetu watu wa Mungu wameitwa na Mungu ili waishi maisha yao kwa njia takatifu huku wakiwa dhabihu zilizo hai; "Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu" (Warumi 12:1-2). Ibada ya kiroho sio tu ukosefu wa ala za muziki kanisani, bali ni uwepo wa Roho Mtakatifu, jambo ambalo linatokana na mtu kuisha maisha mtakatifu. Basi ni ombi letu kwamba roho zetu zitashikamana na muziki wa mbinguni, na kwamba urembo wa muziki wetu utokane na mioyo yetu iliyojaa neema yake Mungu. Basi hebu daima tuwe mawe yaliyo hai, nyumba ya kiroho, na ukuhani mtakatifu ambao unatoa sadaka za kiroho ambazo zinampendeza Mungu kupitia kwakee Yesu Kristo (1 Petro 2:5). ■

# Mwongozo wa Biblia

Kuabudu katika Roho na Kweli. —Yohana 4:23-24

Mkisemezana kwa Nyimbo. —Waefeso 5:19

Mkifundishana na kuonyana kwa Zaburi. —Wakolosai 3:16

Mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu. —Wakolosai 3:16

Mkiimba kwa Roho na kwa Akili. —1 Wakorintho 14:15

Kumshangilia Bwana mioyoni mwenu. —Waefeso 5:19



# Maswali na Majibu

## Je, matumizi ya ala za muziki katika ibada ili kumsifu Mungu ni dhambi?

Kwa kweli kutumia ala za muziki sio dhambi; lakini kulingana na Maandiko na pia kulingana na historia ya kanisa matumizi ya ala za muziki katika ibada za sifa si njia muafaka au inayokubalika ya kumwabudu Mungu. Lakini tunahitaji kuwa makini ili tusimlaani kila mtu ambaye anatumia ala za muziki kwa sababu watu tofauti wanaweza kuwa na mwanga na ufahamu tofauti kuhusiana na swala hili. Kuna mambo ambayo hayajasemwa kuwa aidha ni dhambi au sio dhambi, lakini lengo la watu wote wanaomtafuta Mungu kwa bidii linastahili kuwa kumfuata Yeye kwa karibu na kwa uangalifu mkubwa. Yakobo 4:17 inasema, "Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi." Ikiwa mtu atajua na kuelewa ukweli huu kupitia kwa Roho Mtakatifu halafu akatae kubadilisha mienendo yake kwa sababu ya "kupenda ala za muziki" basi hiyo ni dhambi, kwa sababu ni uasi unaotoka moyoni mwake. Kumwabudu Mungu bila kutumia vifaa vya muziki ndio njia iliyo kamili zaidi. Wale ambao hawafuati njia hii ya ibada wanaishi kwa kiwango duni zaidi kuliko kile ambacho tumepewa katika Agano Jipya na watu kama hao wanajinyima baraka kuu zaidi ya kufanya ibada ya kweli ya kiroho. —mws

## Ni kwa nini hatustahili kufuata maagizo ya Daudi kuhusu kumwabudu Mungu kwa kutumia ala za muziki hata ingawa Daudi alisemwa na Mungu kuwa ni "mtu anayeupendeza moyo wangu"?

Maandiko yote yanastahili kutafsiriwa na kutumiwa kulingana na kipindi ambacho yaliandikwa. Katika Zaburi 144:1 tunasoma kwamba Daudi alisema kwamba, "Na ahimidiwe Bwana, mwamba wangu, anifundishaye mikono yangu vita, vidole vyangu kupigana." Ni kweli kwamba Mungu alimbariki Daudi katika mapigano na vita ambavyo alishiriki na akamsaidia kuuua na kuangamiza maadui zake, lakini jambo hilo ni ngeni kabisa katika wakati huu wa Injili. Sasa Mungu anatutaka kuachana na vita na mapigano, kuwapenda maadui zetu, kuwafanyia wema wale ambao wanatuchukia na wanaotutumia vibaya kwa njia ya madaharau, na hata akatwambia "Msishindane na mtu mwovu" (Mathayo 5:38-45). Mungu pia alimruhusu Daudi kuwa na wake wengi na akambariki na kubariki uzao uliopatikana kutokana na wake hao. Lakini katika kipindi hiki Mungu amelaani matendo hayo na kamwe Yeye hatabariki yeyote ambaye anafuata mfano huo wa Daudi. Ndiposa tunasema kwamba Maandiko yanahitaji kutafsiriwa na kutumiwa kulingana na kipindi chake. Jambo hilo linaonekana kuwa ni kweli katika Zaburi 150:3-8 na hata katika Zaburi zingine ambako kunasemwa kuhusu matumizi ya ala za muziki au uchezaji wa rumba (densi) kama ibada kwa Mungu. Lakini hakuna andiko hata moja la Agano la Kale ambalo linaweza kubatili kanuni au mafundisho ya Agano Jipya kwa sababu Agano Jipya ndilo "agano bora zaidi," na ndilo ambalo Mungu anataka tuishi kwalo.

Ni kweli kwamba katika siku zake Daudi alikuwa "mtu anayeupendeza moyo wangu (Mungu)" lakini yule ambaye ataupendeza moyo wa Mungu katika siku zetu anahitaji kuishi kwa kiwango cha hali ya juu zaidi kuliko cha Daudi na ambacho Daudi hakuwahi kupata nafasi ya kukijua. —Harlan Sorrell

## Katika Warumi 15:9 na Yakobo 5:13 neno *kuimba* limetafsiriwa kutoka kwa neno la lugha ya Kiyunani *psallo*. Je, Maandiko hayo ya Agano Jipya yanaunga mkono matumizi ya ala za muziki?

La, hasha. Maandiko hayo hayaungi mkono au kutoa maagizo ya matumizi ya ala za muziki. Matumizi ya neno *psallō* yameleta mgogoro kwa sababu maana ya neno hilo katika karne tofauti tofauti imebadilika. Maana moja ambayo inatokana na miundo ya lugha ya Kiyunani ni sauti ya *twang'* kama ile inayofanywa na vyombo vya muziki kama vile gita wakati mtu anapoguza nyuzi zake zilizokazwa. Walakini, maana ambayo imetolewa na wasomi stadi wa lugha za Biblia inaonyesha kwamba neno hilo linapotumika katika Agano Jipya linakuwa na maana ya "kuimba."

Kamusi ya Agano Jipya ya Kiyunani-Kizungu na ambayo inahusiana na miundo ya lugha (*Thayer's Greek-English Lexicon of the New Testament*) inasema kwamba katika Agano Jipya psallō ni neno ambalo linaashiria "kuimba tenzi, kusherehekea sifa za Mungu kwa wimbo." Vile vile kamusi fafanuzi ya Vine ya maneno ya Agano Jipya (*Vine's ExpWository Dictionary of the New Testament Words*) inatoa maana ya kale ya neno hilo psallō halafu inasema kwamba "Katika Agano Jipya maana yake ni kuimba wimbo, kuimba sifa." —mws

JE, **WAJUA?**

*Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu.* —Ufunuo 5:8

Kitabu cha Ufunuo ni kitabu cha mifano na pia ni kitabu ambacho kinachora mchoro mzuri wa watakatifu wakizunguka kiti cha enzi huku wakiwa na vinubi mikononi wakiimba wimbo wa ukombozi. Lakini vinubi hivyo vya mbinguni sio vinubi vya kawaida bali ni mfano wa sifa ambazo Mungu hupewa na watu wake. Maana ya mfano huo ni umoja ambao unapatikana kutokana na watakatifu kuwa na umoja na maelewano ya karibu na Roho Mtakatifu.

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# KAZA KAMBA KWENYE VINUBI VYAKO

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana

"Kazeni kamba za vinubi vyenu enyi nyinyi kundi kubwa
mliokombolewa ili kumtukuza Kristo.
Hebu imbieni jina lake lililofungua mlango wa rehema;
Tazama ni muziki mtamu kwa wenye dhambi waliopotea,
Mziki wa kupendeza kwa watakatifu milele na milele."

—Warner, Danieli.
Muziki wa Jina Lake (*The Music of His Name).*

Kabla ya muziki ambao unatumia ala nyingi za muziki kwa pamoja (yaani sinfonia) kuanza kuchezwa wanamuziki hukaza kamba za ala zao ili ala hizo ziweze kuwa na umoja wa konsati na ndiposa muziki huo usikike kuwa ni sauti moja. Sauti ya ala hizo za muziki itasikika kuwa haina umoja ikiwa kila mushiriki wa sinfonia hiyo atakaza kamba za ala zake za muziki na kuzifanya kuwa na viwango tofauti tofauti vya kutoa sauti. Ni wakati tu sauti za ala hizo za muziki zinapolingana na sauti za ala za muziki (za kiongozi wao) ndipo sauti yao wote husikika kuwa na urembo mkuu.



Wakati watu wamekusanyika kumwabudu Mungu linakuwa ni jambo muhimu sana kwamba kila mtu awe ameandaa moyo wake ili uwe na umoja na Roho Mtakatifu wa Mungu; ndiposa mwandishi ambaye ananukuliwa hapo juu anasema "kazeni kamba za vinubi." Wakati wa ibada ni wakati ambapo Wakristo huacha mambo yanayowasubua maishani na kwa pamoja wanamtukuza Kristo. Ikiwa kusanyiko halina utangamano na Roho Mtakatifu basi haitakuwa budi kwamba sauti ya ibada yake hazitakuwa na umoja.

Umoja wa Roho hupatikana kutokana na mioyo ambayo imekarabatiwa na kufikia kiwango cha Bwana wao. Na itakuwa ni faida kubwa kwa ibada hiyo ikiwa viongozi wake watavua mizigo ya maisha yao ili mioyo yao na akili zao ziwe na umakini kwa Roho Mtakatifu. Jambo hili likifanyika upako utakuwa mkubwa zaidi na kusanyiko hilo linakuwa la kubarikiwa kwa kiwango kikubwa sana kulingana na jinsi Roho Mtakatifu anakavyotembea katikati mwao. "Kazeni kamba za vinubi" ili furaha yenu ndani yake Bwana izidi kukua wakati mnapofanya sifa na ibada kwake. ■